

## **MH. MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO AAGIZA PAWEPO NA MGAO WA MAJI**

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Anna Mghwira ameagiza pawepo na mgao wa maji kati ya Kata ya Toloha na Kata ya Chomvu. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa ameyasema hayo alipo fanya ziara katika kata ya Toloha ikiwa ni mwaliko wa Wananchi wa Kata hiyo ili aweze kuwasikiliza kero waliyo nayo ya maji.

Akizungumza kwa niaba ya Wananchi wa Toloha, Mwenyekiti wa Kijiji cha Simu Kizungo Ndugu Marijani R. Mgonja alieleza kuwa pamoja na kwamba kwa sasa ni kipindi cha ukame lakini tatizo kubwa la maji linatokana na baadhi ya wananchi kujiunganishia maji kwenye eneo la milimani (Kata ya Chomvu) ambako ndiko chanzo cha maji kilipo. Pia ukosefu wa maji unatokana na kufanya shughuli za binadamu kama kilimo na kukata miti kwenye eneo la chanzo cha maji.

Mjumbe wa Serikali ya Kijiji ambaye pia ni mjumbe wa Bodi ya maji Toloha Ndugu Rashid Rajab alieleza kuwa ***“Mimi nilitembelea kwenye chanzo cha maji na kukuta shughuli nyingi za kibinadamu zinaendele pamoja na watu binafsi kujiunganishia maji”***.

Baada ya kuwasilisha kero zao, Mh. Mkuu wa Mkoa alitoa maagizo kwamba kutokana na umuhimu wa maji ni lazima kuanzia sasa pawepo na mgao ambapo wananchi wa Toloha walikubaliana na uamuzi huo na kushauri kuwa wao wapatiwe mgao usiku na Chomvu wapatiwe mgao wakati wa mchana.

Mheshimiwa RC alisisitiza kuwa shughuli zozote za uharibifu wa mazingira zinazoendeshwa kwenye chanzo cha maji na kwenye maeneo ya **“Intake”** zisitishwe mara moja sambamba na wale waliojiunganishia maji kuhakikisha kuwa hawaendelei kujiunganishia maji tena ili maji yawepo ya kutosha.

Endapo zoezi la mgao wa maji litafanikiwa itasaidia wananchi wa Toloha wenye jumla ya Kaya 803 kuepuka kwenda kufuata maji umbali mrefu ambapo kwa sasa wanapata maji kutoka Kata ya Jirani ya Kwakoa na maji haya wanayapata kwa kununua.



***Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro akiwa anasikiliza Wananchi wa Kata ya Toloha alipowatembelea tarehe 12.02.2018. (Picha na Eliakimu E. Kimuto)***